SHULE YA AWALI NA MSINGI THEMI HILL
KAZI YA LIKIZO
KISWAHILI DARASA LA VII - 2020

JINA: _____ DARASA_____ TAREHE_____

SEHEMU A: SARUFI

1. Ipi ni sentensi iliyo ukanushi na sentensi "sisi hula wali kila siku
   A. Sisi hulaga wali kila siku
   B. Sisi hatuli wali kila siku
   C. Sisi hatulagi wali kila siku
   D. Sisi hatuna kula wali kila siku
   E. Sisi twala wali kila siku

2. Bidhaa zimeadimika madukani siku hizi kitenzi katika sentensi hiyo ni .....
   A. Bidhaa
   B. madukani
   C. Siku
   D. Zimeadimika
   E. Siku hizi

3. Mzungu alisema kwamba Tanzania ni nchi nzuri kivumishi kwenye sentense hiyo ni .....
   A. Mzungu
   B. Nzuri
   C. Tanzania
   D. Nchi
   E. Kwamba

4. Tendo katika neno wamegoma ni .....
   A. Wa
   B. Me
   C. Goma
   D. Gom.....
   E. .....a

5. Wale ni watoto wema. Neno wale katika sentensi hiyo limetumika kama.....
   A. Kiwakilishi
   B. Nomino
   C. Kioneshi
   D. Kiunganishi
   E. Kivumishi

6. Nilikuwa ninafanya mazoezi. Neno "Nilikuwa" katika sentensi hiyo limetumikakama aina ipi ya vitenzi?
   A. Shirikishi
   B. Kikuu
   E. Kisaidizi
   C. Halisi
   D. Kutenda

7. Msakamali alikuwa mkulima wetu hodari. Katika sentensi hiyo neno lipi ni kitenzi kishirikishi?
   A. Wetu
   B. Mkulima
   C. Alikuwa
   D. Hodari
   E. Wetu hodari

8. Baba na mama watasafiri kesho asubuhi. Kifungu cha maneno “kesho asubuhi ni.....
   A. Kielezi
   B. Kivumishi
   C. Kiunganishi
   D. Wakati
   E. Kitenzi

9. La kuvunda halina ubani,sehemu ya sentensi iliyopigiwa mstari ni aina ipi ya kiwakilishi?
   A. Cha sifa
   B. Cha kuonesha
   C. Cha kumiliki
   D. Cha A-unganifu
   E. Cha kurejesha

10. Ramla ni msichan anyesoma shule ya msingi Mapinduzi. Sentensi hiyo iko kama nafsi gani?
   A. Nafsi ya pili umoja
   B. Nafsi ya kwanza umoja
   C. Nafsi ya tatu wing
   D. Nafsi ya pili wingi
   E. Nafsi ya tatu umoja

11. Lo! Na wewe umekuja! Neno lililopigiwa mstari ni aina gani ya maneno
   A. Kiwakilishi
   B. Kihisishi
   C. Kiigizi
   D. Kivumo
   E. Kiunganishi

12. Neno lipi halihusiani na mengine kati ya yafuatayo
   A. Nomino
   B. Kitenzi
   C. Kishiriki
   D. Kiunganishi
   E. Kihisishi

13. Ongea kwa sauti kwani sikusikii vizuri. Maneno yaliyopigiwa mstari yametumika kama aina ipi ya maneno?
   A. Kielezi
   B. Kiunganishi
   C. Nomino
   D. Kihisishi
   E. Kivumishi

14. Mtahudhuria mafunzo mwaka mzima. Sentensi hiyo ni ya nafsi gani?
   A. Nafsi ya kwanza wingi
   B. Nafsi ya pili wingi
   C. Nafsi ya tatu wingi
   D. Nafsi ya pili umoja
   E. Nafsi ya tatu umoja

15. Yule msichana ameumbika kama malaika. Sentensi hiyo ni ya kauli ipi ya mtendaji.
   A. Kutendwa
   B. Kutendea
   C. Kutendana
   D. Kutenda
   E. Kutendeka

16. Mgonjwa amepata <u>nafuu</u>. Neno mbadala linaloweza kutumika mahali pa nenonafuu ni .....
    A. Mafua
    B. Ukuu
    C. Homa
    D. Ahueni
    E. Afadhali

17. Kinyume cha “inama” ni kipi?
    A. Inuka
    B. Bendi
    C. Nyooka
    D. Simama
    E. Geuka

18. Neno lipi kati yayafuatay lipo katika ngeli ya A-WA
    A. Ukuta
    B. Shati
    C. Simu
    D. Kalamu
    E. Kunguni

19. Mtu ufanyanye kazi ya fundi magari anaitwa.....
    A. Fundi hodari
    B. Fundi gereji
    C. Makanika
    D. Kondakta
    E. Taniboi

20. Neno lipi kati ya yafuatayo lina maana karibu sawa na neno “hitilafu”
    A. Kasoro
    B. Halafu
    C. Hata
    D. Kalifu
    E. Lakini

21. Vipindi vya masomo shuleni kwetu humalizika alasiri. Katika sentensi hiyo kielezi ni:-
    A. Vipindi na masomo
    B. Shuleni na kwetu
    C. Humalizika na masomo
    D. Shuleni na alasiri
    E. Kwetu na alasiri

22. Kwa kawaida watu wengi hutumia mkono wa kuume kufanyia kazi. Mkono wa kuume ni:-
    A. Mkono wa pili
    B. Mkono w akulia
    C. Mkono wa mwanaume
    D. Mkono wa kushoto
    E. Mkono ni mkono

23. Sherehe ya kuagana itafanyika mtondogoo. Maana yake sherehe itafanyika:-
    A. Kesho
    B. Jana
    C. Siku ya nne baada ya leo
    D. Kila baada ya siku chache
    E. Siku baaya ya kesho

24. Huyu .....aliyemwokoa yule msichana kutoka mtoni alikokuwa ametumbukia.
    A. Ndio
    B. Ndiye
    C. Ndiyo
    D. Ni
    E. Ndipo

25. Bila shaka katiba mpya itapatikana mwakani. Maneno mawili ambayo ni nomino .....
    A. Mpya na mwakani
    B. Shaka na katiba
    C. Mwakani na bila
    D. Bila na mpya
    E. Katiba na itapatikana

26. Wanakijiji walimsaka simba. Nini maana ya kumsaka?
    A. Walimtafuta kwa bidii zote
    B. Walimkimbiza vichakani
    C. Walimwacha tu akaondoka
    D. Walimngoja atokeze
    E. Walimtega kwa mtego

27. Uzani wa Maria ni mkubwa kuliko wa Mwanaidi. Maana ya uzani ni:-
    A. Urefu
    B. Uzito
    C. Uzuri
    D. Unene
    E. Ukubwa

28. Kamilisha sentensi ifuatayo kwa neno stahili " Aliwaogesha watoto..... akawavika nguo safi.
    A. Kisha
    B. Kabla ya
    C. Kuliko
    D. Licha ya
    E. Kwa sababu ya

29. Mwalimu ni kwa kufundisha na .....nikwa kuwinda. Kamilisha sentensi kwa neno sahihi
    A. Simba
    B. Mshale
    C. Mchungaji
    D. Msasi
    E. Mbwa

30. Kinyume cha hatari ni .....
    A. Holota
    B. Salama
    C. Salimini
    D. Ubaya
    E. Ukweli

31. Kuku jike huitwa .....
    A. Mtetea
    B. Koo
    C. Jimbi
    D. Jike

32. Mwalimu alitahadharisha kwamba uhuru wa kujieleza usivunje sheria. Neno "alitahadharisha lina maana ya .....
    A. Alionya
    B. Aliwezesha
    C. Alihatarisha
    D. Alituambia
    E. Alionesha heshima

33. Mtama na mpunga umewekwa kwenye ungo. Ni yupi katika ya viumbe wafuatao watatokwa na mate kwa hamu ya kula wakiuona?
    A. Ng'ombe
    B. Panzi
    C. Fisi
    D. Bundi
    E. Kwelea kwelea

34. Lipi kati ya maneno yafuatayo halihusiani na mengine
    A. Sharafa
    B. Masharubu
    C. Kope
    D. Nyusi
    E. Mvi

35. " Nitakuja kukuona kesho" Katika kauali taarifa sentensi hiyo itakuwa:-
    A. Alisema nitakuja kukuona
    B. Nitakwenda kukuona kesho
    C. Alisema atakwenda kumuona siku inayofuata
    D. Kukuona itakuw akesho
    E. Nitakuja kumuona kesho

36. Hati ayako imepotea. Katika sentensi hiyo neno yako limetumika kama:-
    A. Kiwakilishi
    B. Nomino
    C. Kivumishi
    D. Kitenzi
    E. Kiunganishi

37. Juma anaweza kusoma vizuri ingawa ni mvivu kwenda shule. Katika sentensi hiyo lipi kati ya maneno yafuatayolimetumika kama kivumishi?
    A. Mvivu
    B. Vizuri
    C. Ingawa
    D. Anaweza
    E. Juma

38. Nimeazimia kutembea kwa miguu hadi mwisho wa safari yangu. Neno lipi katik a ya yafuatayo lina maana swan a lililopigiwa mstari.
    A. Nimekusudia
    B. Nimekubali
    C. Nimeona
    D. Nimeonelea
    E. Nimekoma

39. Mtoto wa kitukuu ni:-
    A. Mjukuu
    B. Kilembwekeza
    C. Kitukutuku
    D. Mpwa
    E. Mwana

40. Yupi anapenda kucheza mpira wa mikono? Katika sentensi hiyo neno anapend ani aina gani ya kitenzi?
    A. Kitenzi kisaidizi
    B. Kitenzi halisi
    C. Kitenzi kishirikishi
    D. Kitenzi nomino
    E. Kitenzi kiunganishi

SEHEMU B: LUGHA YA KIFASIHI

41. Kamilisha methali ifuatayo "Mfa Maji.....
    A. Hulia
    B. Huomba msaada
    C. Haachi kutapa tapa
    D. Huona kengeza
    E. Hunywa maji

42. Nahau ipi kati ya zifuatazo ina maana sana na "huwezi kitu"
    A. Mwaga unga
    B. Ota mizizi
    C. Shika njia
    D. Hufui dafu
    E. Shika hatamu

43. Ini la ng'ombe huliwa hata na walioko mbali. Jibu la kitendawili hicho ni.....
    A. Kifo
    B. Mkaa
    C. Chupa
    D. Nyayo
    E. Ndegu

44. Pitwa na wakati ina maana.....
    A. Fukuzwa kazi
    B. Kubali kwa maneno
    C. Kufanya mambo kizamani
    D. Kufanya mambo kisasa
    E. Kuchelewa kufanya mambo sawa sawa

45. Ukilianza jambo huwa umelianza vibaya au umelianza vizuri tuu. Ni methali ipi kati ya zifuatazo inashabihiana na maelezo hayo.
    A. Baada ya kidonda msumari wa moto
    B. Baada ya dhiki faraji
    C. Baada ya kisa mkasa
    D. Ukiona vyaelea vimeundwa
    E. Awali ni awali, hakuna awali mbovu

46. Baada ya dhiki faraj au faraji. Methali hii ina maana ipi?
    A. Anayewashwa ndiye anayejikuna
    B. Mapumziko wema na raha huja tu baada ya mtu kutaabika,
    C. Watu hutembea bila viatu lakini wanapodungwa na mwiba hapo wanaanza kukumbuka viatu
    D. Upatapo nafasi nzuri ni lazima uitumie vizuri
    E. Ukifanya kazi japo kidogo tu kila mara utaweza kukamilisha jambo kubwa sana.

47. Lenye mwanzo lina mwisho. Hii ni methali inaylingana katika maana na methali ifuatayo:-
    A. Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha
    B. Leo kwako kesho kw amwenzio
    C. Leo ni kabla ya kesho
    D. Kwenda bure si kukaa bure
    E. La leo litende leo

48. Chupa ni maana ya kitendawili kipi kati ya vifuatavyo:-
    A. Napigwa faini kosa sitini
    B. Watoto wa binadamu wakiondoka hawarudi
    C. Ba funua, ba funika
    D. Ajenga ingawa hana mikono
    E. Nyumba yangu ina mlango juu

49. Shinda majaribu ni nahau inayelezwa vizuri na maelezo yapi kati ya fuatayo:
    A. Epuka vishawishi
    B. Ruka mtego
    C. Kubali jambo
    D. Kataza jambo
    E. Majaribu ni lazima uyashinde

50. Kitendawili “Hana adabu wala staha kwa watu” kinalandana katika jibu na kitendawili kipi kati ya vifuatavyo
    A. Ukitaka kuju aana mbio mwonyeshe moto
    B. Napand amti na kichaa wangu
    C. Kabla hajanitazama nimekwisha mpiga.
    D. Huliogopa sana jua
    E. Akibeba watoto wake hawezi kuwashusha

51. Methali ipi kati ya zifuatazo inayohimiz awazazi wasiogope kuwatia adabu watoto wao wakiwa wadogo ili wasiharibike wanapokuwa watu wazima
    A. Mcheza kwao hutunzwa
    B. Mbio za sakafuni huishia ukingoni

C. Mchelea mwana kulia mwenyewe
D. Kafiri akufanye si Islamu asiyekufaa
E. Kachume juani ule kivulini

52. Kamilisha methali " Fuata nyuki .....
A. Ukose asali
B. Ule uhondo
C. Ule cha mtema kuni
D. Uumwe na nyuki
E. Ule asali

53. Nina saa ambayo haijawahi kusimama tangu itiwe ufunguo. Maana ya kitendawili hiki ni:-
A. Moyo
B. Jua
C. Mbingu
D. Mwezi
E. Maji

54. Maneno bila vitendo hubakia tu kuwa maneno. Maelezo haya yanaieleza vizuri methali ipi?
A. Maneno makali yakata ini
B. Maneno fedha, majibu dhahabu
C. Maneno ni jangwa tembezi
D. Mambo ya ngoma huishia ngomani
E. Maneno matupu hayavunji mfupa

55. Timu ya wanafunzi wa Mtakuja iliposhinda mchezo wa mpira, wanafunzi wote walipiga makofi. Walipiga makofi ina maana:-
A. Walishangilia sana
B. Walipiga kelele
C. Waliimba
D. Walikimbia
E. Walicheza wote

56. Nazi na mkwezi ni jibu la kitendawili.....
A. Kilemba chako haazimishi
B. Bibi hatui mzigo wake
C. Ajihami bila silaha
D. Ubwabwa wa mwan mtamu
E. Amefika kabla mjumbe hajafika

57. Kipara cha babu kinafuka moshi. Jibu la kitendawili hiki ni
A. Sima
B. Chai
C. Maziwa
D. Kiazi
E. Maji moto

58. Nimefagia kiwanja wangu kaja miguu mirefu kauchafua. Kitendawili kina maana.....
A. Miti
B. Barabara
C. Mvua
D. Misitu
E. Njia

59. Kunipa nyama ya ulimi pekee hakutoshi vile vile natak nione vitendo. Kumpa mtu nyama ya ulimi ina maana:-
A. Kumpa ulimi wa mbuzi ale
B. Kumnong'oneza
C. Kumbembeleza
D. Kumwambia maneno mazuri
E. Kumpendelea

60. Mtu akimwambia mwenzake, "utaona kilichomtoa kanga manyoya" ni sawa na amemwambia:-
A. Utakula chumvi nyingi
B. Utakata shauri
C. Utapokelewa kwa mikono miwili
D. Utapewa notisi
E. Utaona cha mtema kuni

SEHEMU C: USHAIRI

A:**Soma shairi lifuatalo na kisha ujibu maswali yanayofuata**

Ushirika ndugu zangu, ndiyo nyenzo ya maisha,
Natoa undani wangu, ukweli kuwaonesha,
Nyuki, siafu na chungu, wajua yao maisha,
Hivi vidudu vya Mungu, shirika vyatufundisha.

Umewahi kuwaona, chungu wanvyotembea,
Mstari wapangana, wakiend akuhemea,
Na mchwa wakikutana, vita kubwa hutokea
Mzigo wabebeshana, nymbani wakirejea.

Umewahi kuwaona,, mchwa wakiwa kazini,
Kazi wanavyogawana, wagawana vikundini,
Akili wala hawana, kama za kwetu kichwani
Chuguu utaliona, kama mnara angani.

Chunguza tena siafu, waishivyo kwa umoja,
Hata mzoga wa pofu, utaisha siku moja,
Wamvamia sifufu, kipande moja kwa moja,
Waongozana kwa safu, nyumbani kuleta tija.

MASWALI

61. Kichwa kinachofaa shairi hili ni:-
    A. Mchwa, siafu na nyuki
    B. Mchwa, nondo na siafu
    C. Ushirikiano wa siafu na chungu
    D. Ushirikiano wa wadudu
    E. Mchwa na kichuguu chake

62. Mstari katika shairi huitwa.....
    A. Arudhi
    B. Kina
    C. Mshororo
    D. Mstari mnyofu
    E. Mizani

63. Vina vya ubeti wa nne vya kati na mwisho ni
    A. na na ka
    B. fu na ja
    C. ja na ni
    D. na na fu
    E. u na chu

64. fundisho la shairi hili ni.....
    A. jinsi wadudu wanavyogawana kazi
    B. umuhimu wa ushirikiano
    C. maisha ya nyuki mzingani
    D. siafu na nyuki wanvyofanya kazi
    E. bidii ya mchwa kazini

65. Neno “tija” kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana.....
    A. Matokeo yenye manufaa
    B. Kujitayarisha

C. Ziada

D. Taji dogo na jepesi

E. Liojaa kwa wingi

B: Soma shairi lifuatalo na kisha jibu maswali 66 – 70

Mazingira ni uhimu, kwetu sisi binadamu,
Usije kuyahujumu, viumbe utadhulumu,
Ni letu sote jukumu, mazingira kuhudumu,
Tuyatunze mazingira, ili nayo yatutunze

Chakula nayo makazi, mazingira tupatia,
Hewa safi kama kazi, yote tunajivunia,
Hata kama kiangazi, maji tunajipatia,
Tuyatunze mazingira, ili nayo yatutunze

MASWALI

66. Shairi hili linatoa ujumbe gani?
    A. Tuyatunze mazingira
    B. Mazingira ni muhimu
    C. Tuhujumu mazingira
    D. Yatutunze mazingira
    E. Sisi binadamu

67. Mshairi ama maana gani anayesema “Usije kuyahujumu?”
    A. Usiyaharibu mazingira
    B. Usiyadhulumu mazingira
    C. Usiyahudumu mazingira
    D. Usiyaache
    E. Usiyaache mazingira

68. Jukumu la kuyatunza mazingira ni la .....
    A. Wanamazingira
    B. Wataalamu
    C. Wakulima
    D. Wafugaji
    E. Kila mtu

69. Ubeti wa mwisho umetaja mambo makuu manne ambayo mazingir ayanaweza kutupatia. Ni yapi hayo?
    A. Maji, udongo, hewa na miti
    B. Chakula, makazi, hewa na maji
    C. Udongo, wanyama, chakula na nyumba
    D. Hewa, chakula, maji na mimea
    E. Udongo, hewa, maji na mashamba

70. Ubeti wa kwanza mshororo wa pili msanii anasema, usije kuyahujumu, viumbe utadhulumu. Ukiyahujum mazingira viumbe watudhulumikaje?
    A. Watakosa mahali pa kuishi
    B. Wataangamia
    C. Watataabika
    D. Watakimbia
    E. Watajificha

SEHEMU D: UTUNGAJI

A:Sentensi zifuatazo haziko katika mtiririko mzuri wa mawazo. Zipange vizuri kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E ili zilete mtiririko mzuri wa mawazo.

71. Kwanza unatupa mwanga wakati wa usiku
72. Kama moto usingegunduliwa, maisha yawatu yangekuwa duni.
73. Moto una faida nyingi san akwa binadamu
74. Katika miji yenye viwanda, moto wa umeme ndio unaotumika katika kuendesha mashine na mitambo mbalimbali.
75. Tangu moto ulipogunduliwa maisha ya mwanadamu yameendelea kubadilika siku baada ya siku.

B:Panga sentensi zifuatazo katika mtiririko unaofaa kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E

76. Watoto wawili wakamwona wakapiga yowe
77. Akaiba saa za mkono zenye tahmani kubwa
78. Mwizi alivunja kioo cha duka lililojaa bidhaa
79. Wakatokea watu wengi na askari wakamkamata na kumpeleka kituo cha polisi
80. Mwizi aliposikia makaripio akatimua mbio

SEHEMU E: UFAHAMU

A: Soma kifungu kifuatacho cha habari na kisha jibu maswlai yanayofuata.

Siku zote wamekuwa wakiishi katika mazingira yanayozunguka makazi ya binadamu. Walijiita kuwa wao eti ni rafiki “Chanda na pete” wa binadamu. Urafiki wao ulianza pale binadamu alipoamua mwenyewe bila kufahamu kuwa anamtengezea mbu maskani ya kudumu. Urafiki huo ulijaa mashaka kwa kila mmoja wo. Hasa wakati wa mvua za masika pale binadamu alipotupa takataka ovyo.

Hizi ni takataka kama vile makopo, vifuu vya nazi, vigae vya vyungu, vikombe na sahani. Pia kuchimba mashimo yanayoweza kutuamisha maji mengi na kuacha nyasi zikizagaa na kurefuka ovyo ovyo karibu na nyumba yake.

Kwa kufanya hivyo, mbu walifurahia sana kwani waliweza kuzaliana kwa wingi. Binadamu aliona ni hali ya kawaida kwa kuwa anashikilia usemi usemao “Hakuna masika yasiyokuwa na mbu.” Aghalabu mbu wamekuwa wakinong’ona katika masikio ya binadamu. Walimsisitizia kuwa aendelee kumwaga maji machafu katika vishimo na vyombo vibovu vibovu nje. Walidai kwamba vijidudu vinavyoishi ndani ya maji hayo machafu vinafaa kwa chakula ni kama samaki. Akiendelea kumlaghai amfungulie mlango na madirisha waishi pamoja, hasa wakati wa kiangazi maji yanapokauka. Lengo wapate msaada wa chakula.

Lakini binadamu hakupenda kusikiliza maneno ya mbu, yeye aliamua kufukuza mbu wote nyumbani mwake na kuwaambia wasirudi tena. Hali hii imezua vita kubwa kati yao. Hasa, baada ya mbu kuingia ndani ya nyumba kwa nguvu na kugundua hakuna kitakachofaa kujikimu humo ndani zaidi yadamu ya binadamu.

Usiku unapoingia mbu makundi makundi humnyonya binadamu damu yake na kumwekea vijidudu walivyonavyo. Hivyo, binadamu hushikwa na homa kali, kutapika, kuumwa kishwa na wakati mwingine kuaga dunia. Wanadamu wataalamu wanathibitisha kuwa hali hiyo inaitwa ugonjwa wa Malaria.

Basi ili kuondokana na adha hiyo, binadamu anashauriwa kukataa urafiki na mbu. Atunze mazingira yake kwa kufukia mashimo na taka zote zinazotuamisha maji machafu.

Pia kutumia chandarua chenye dawa kuzuia mbu wabishi wanaoingia ndani anapokuwa amelala na mwisho kwenda zahanati mara napoona dalili zilizotajwa. Binadamu wote kwa pamoja wanashauriwa washiriki katika kutunza mazingir aili waweze kumwangamiza kabisa mbu. Kwa kufanya hivyo inawezekana wakaishi bila kuugua ugonjwa wa malaria na Taifa lao halitapoteza nguvu kazi kubwa kwa kupitia janga hili.

MASWALI

81. Unafikiri mwandishi wa habari hii anasema ni watu gani ambao siku zote wamekuwa wakiishi katika mazingira ya makazi ya binadamu?
82. Binadamu anamtengenezea mbu maskani ya kuishi ya kudumu kwa vipi?
83. Unafikiri vijidudu vinavyoishi ndani ya maji machafu anayovieleza mwandishi ni vijidudu gani?
84. Ni hali ipi anavyoieleza mwandishi ambayo imezua vita kubwa baina ya binadamu na mbu?
85. Mwandishi anamshauri binadamu kukataa urafiki na mbu. Afanye nini?

B: Soma kifungu kifuatacho cha habari na kisha ujibu maswali 86 – 90 kwa ufupi

UKIMWI ni ugonjwa hatari usio na kinga wala tiba. UKIMWI ni kifo. Mgonjwa wa UKIMWI hawezi kupat dawa za kumponyesha. Mgonjwa huyo huweza kupat adawa za kurefusha maisha. Baada yamuda usiofahamika mgonjwa hufa. UKIMWI huenezwa kwa njia mblimbali. Kati ya hizo nikuchangia vitu vyenye ncha kali, miswaki nakujamiiana.
Nyingine ni kuongezwa damu yenye virusi vya UKIMWI. Mtu anaweza kufahamu kama ana virusi au la kwa kupima afya yake hospitali. Yeye aliyegundulika kuwa ameathirika awe an nidhamu asiwaambukize wengine.
Asiyeathirika ajitunze asije kuambukizwa na wengine. Hali hii itapunguza maambukizi mapya ya UKIMWI.

MASWALI

86. Mwandishi amesema kuwa UKIMWI ni kifo. Kwa sababu gani?
    _____
87. Mwandishi ameeleza kuwa mgonjwa wa UKIMWI hawezi kupata dawa ya kumponyesha bali anaweza kupata dawa gani?
    _____
88. Mwandishi ametaja njia nne ambazo kwazo UKIMWI huenezwa. Ni zipi hizo?
    _____
89. Kwa nini ni jambo zuri kwa mgonjwa wa UKIMWI kuwa na nidhamu?
    _____
90. Mwandishi amesema, “Hali hii itapunguza maambukizi mapya ya UKIMWI? Ni hali ipi hiyo anayoisema mwandishi?
    _____